RUBYA HEALTH TRAINING INSTITUTE
JOINING INSTRUCTIONS

Tarehe: ……./…../2017

TAARIFA MUHIMU KUHUSU CHUO.

Mpendwa Mzazi/Mlezi/Mfadhili wa: ……Hongera sana mwanao amechaguliwa kujiunga na kozi ya…….

1. a) Taasisi hii ni mali ya Jimbo Katoliki la Bukoba, ambayo imeidhinishwa na kusajiliwa na Wizara ya Afya, maendeleo ya Jamii, jinsia, Wazee na watoto.Vyuo chini ya taasisi hii vimesajiliwa na mabaraza husika na vinatoa mafunzo yafuatayo:stashahada ya uuguzi na ukunga,sayansi ya maabara, afisa tabibu na ngazi ya cheti.Pia taasisi inatoa mafunzo ya mwaka mmoja kwa wahudumu wa afya(Community Health)Taasisi imesajiliwa na NACTE kwa namba:REG No.HAS/017,pia taasisi imepata ithibati(accreditation) yaNACTE.

   Sifa za kujiunga katika taasisi ni kama zilivyoainishwa kwenye jedwali

S/N	KOZI	ALAMA HUSIKA	MUDA
1.	Stashahada ya uuguzi na ukunga.(Diploma)	Biologia C,Kemia C,Fizikia D, Kiingereza D	Miaka 3
	Stashahada ya uafisa tabibu (Diploma)	Biologia C,Kemia C,Fizikia D,Kingereza D,Hesabu D.	Miaka 3
	Stashahada ya sayansi ya maabara (Diploma)	Biologia C,Kemia C,Fizikia D,Kingereza D,Hesabu D	Miaka 3
2	Astashahada ya uuguzi na ukunga (Cheti)	Biologia C,Kemia C,Fizikia D, Kiingereza D	Miaka 2
	Astashahada ya uafisa tabibu(Cheti)	Biologia D,Kemia D,Fizikia D,Kingereza D,Hesabu D	Miaka 2
	Astashahada sayansi ya maabara(Cheti)	Biologia D,Kemia D,Fizikia D,Kingereza D,Hesabu D	Miaka 2
3	Afya ya jamii(Community Health)	Biologia D na vipindi vingine vitatu ufaulu wa D	Mwaka 1

   c) Mwanachuo baada ya kufuzu masomo yake atasajiliwa na mabaraza husika: wauguuzi na wakunga (TNMC),Sayansi za maabara (TML), Afisa tabibu (TMB), Watoa huduma wa afya (watasajiliwa na halmashauri ya wilaya)
   d) Kwako Mzazi/Mlezi/Mfadhili ushirikiano ni muhimu sana ili mwanao aweze kufuzu masomo yake kwa muda uliopangwa.

2.LENGO

Kuwandaa wanachuo, katika elimu, kuwalea katika maadili mema na kuwaelekeza katika utendaji kazi ili waweze kuwa watoa huduma bora kwa manufaa ya jumuiya nzima, Taifa la Tanzania na ulimwengu mzima. NIDHAMU INAZINGATIWA.

3. **MAHITAJI MUHIMU YA MWANACHUO**.

Mwanachuo kabla ya kuanza masomo lazima awe na vifaa hivi vifuatavyo:-

A. VIFAA VYA MASOMO:-

- Kamusi ya kingereza
- Kamusi ya ukunga au Shs. 25,000/=/Kamusi ya Uuguzi au Shs. 25,000/=
- Futi kamba(Tape measure) na rula
- Kalamu za rangi kwa ajili ya kuchora
- Kalamu za wino za kutosha (blue, red na green)
- Madaftari ya kutosha

B. VIFAA VINGINE.

a) Nyenzo za kusalia katika dhehebu lako – Biblia, Rosari, chuo kidogo cha sala, na vitabu vya nyimbo ni lazima kwa wakatoliki.
b) Chandarua (Mviringo)4*6
c) Blanketi 2
d) Mashuka matatu yenye upana na urefu wa kutosha kufunika godoro (Urefu mita 2½ na mita 1½ upana) 4
e) Night dress/Pajama 2
f) Shimizi 2 zenye urefu usawa wa magoti
g) Chupi walau 4 na (skin tight walau 2 kwa wasichana)
h) Taulo 2
i) Viatu vyeusi/kahawia vilivyofunikwa, viwe vya ngozi jozi 2
j) Soksi jozi 2 nyeupe(wasichana),Jozi 2 nyeusi(wavulana)
k) Mwavuli au koti la mvua 1
l) Ndoo ya plastic yenye mfuniko ya lita 20
m) Matumizi ya lazima kama sabuni, mafuta, vibanio vya nguo, kitana kioo n.k.
n) Tochi yenye betri (kwa ajili ya dharura).
o) Jezi ya michezo(Kijani/Bluu)

C: **Vifaa Vifuatavyo ni Kwa Kozi ya Maafisa Tabibu (CO) na Sayansi ya Maabara :**

1. Blood presure machine, Stethoscope, thermometer, Clinical Torch and Box of clean gloves.

4. Mwanachuo awapo chuoni atazingatia utaratibu wa chuo kama atakavyoelekezwa.
5. Tarehe ya kufungua chuo ni **09/10/2017** kwa kozi ya **Uuguzi na Ukunga(Nursing) na Wahudumu wa Afya (Community Health).**

   23/10/2017 kwa kozi ya **Afisa Tabibu (CO)** na **Sayansi ya Maabara** (**LAB**.) ni kati ya saa mbili (2 asubuhi hadi saa nane 8 mchana). Mwanafunzi afike akiwa na mzazi/mlezi au mmoja kati ya jamaa walioorodheshwa na mzazi. (Angalia uk wa 9 Kanuni za Chuo).

6. **Afike na Cheti Halisi cha Kidato cha Nne/Sita (Academic Certificate) na cheti halisi cha Ubatizo, Cheti cha kuzaliwa(Birth certificate) na Pay-In-slip.**

TUNAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA.

KARIBU SANA.

……

MKUU WA TAASISI

RUBYA HEALTH TRAINING INSTITUTE
P.O. Box 133, RUBYA – BUKOBA
TANZANIA - EAST AFRICA
E-mail: info@rhti.ac.tz

...../...../2017

KANUNI ZA TAASISI

UTANGULIZI.

Kanuni hizi ni utaratibu unaotakiwa kuzingatiwa na kufuatwa na kila mwanachuo wakati wote awapo hapa chuoni. Mwanachuo na mzazi au mlezi sharti wazisome kwa makini na endapo watakubaliana nazo wote, basi waweke saini mahali panapohusika. (angalia uk.9)

Matokeo ya mwanachuo kukiuka (kuvunja) kanuni hizi ni kusimamishwa masomo kwa muda, kuachishwa masomo (kufukuzwa) au adhabu nyingineyo inayolingana na uzito wa kosa.

Kanuni hizi zimekusudia kumfaa mwanachuo pamoja na jumuia nzima ya chuo na kumuandaa awe mtoa huduma bora wa afya kwa manufaa ya jumuiya nzima, Taifa la Tanzania na ulimwengu kwa ujumla.

A. KUFIKA CHUONI.

1. Mwanachuo sharti afike chuoni tarehe iliyoandikwa kwenye fomu ya maelezo. Vile vile mwanachuo sharti aripoti tarehe aliyoandikiwa ya kurudi toka likizo. Endapo itabidi achelewe, sharti aje na barua ya kiongozi husika mfano: kama ni mgonjwa, barua ya mganga ikiwa na saini na muhuri wa kituo alichotibiwa, matatizo ya nyumbani barua ya Mwenyekiti wa kijiji. Vinginevyo atarudishwa nyumbani kutafuta uthibitisho.

2. Mwanachuo ajapo chuoni kuanza masomo, sharti aje na cheti cha Afya kilichojazwa na Mganga wa kituo aliyempima kwenye hospitali inayotambulikana, awe ameweka saini, cheo chake na muhuri wa Hospitali.

3. Mwanachuo ajapo chuoni kuanza masomo afike na **KARO YA MUHULAANAOUANZA** na vifaa vyote vinavyotakiwa kwa mujibu wa fomu ya maelezo

4. Mwanachuo ajapo chuoni kwa mara ya kwanza sharti afike na Mzazi/mlezi au jamaa aliyeteuliwa na mzazi (angalia ukurasa wa 9).

B. MAHUDHURIO:

1 Mwanachuo sharti ahudhurie masomo yote na shughuli zote za kimasomo ndani na nje ya madarasa na hospitali.

2 Mwanachuo sharti afanye kazi zote za masomo (Assignments) anazopewa na walimu na kuzirudisha kwa Mwalimu mhusika katika muda unaotakiwa, Vinginevyo atapewa adhabu zifuatazo: - Kwa mara ya kwanza atapewa onyo la maandishi na nakala itatumwa kwa Mzazi/ Mlezi/ Mfadhili, mara ya pili atasimamishwa masomo kwa muda, mara ya tatu ataachishwa masomo.

3 Ni marufuku kwa mwanachuo, kusuka nywele, kupiga kelele au soga ,kucheza karata, wakati wa kujisomea darasani,maktaba, awapo bwenini, bwaloni na hospitalini.

4 Ieleweke kuwa shughuli za kujitegemea, kama vile usafi wa mazingira, kulima bustani kujitolea kusaidia shughuli za chuo ni sehemu muhimu katika kumuandaa mwanachuo.

5 Mwanachuo atashiriki michezo iliyopangwa nataasisi ili kutunza afya na kujenga uhusiano mwema na wenzake.

C. MAVAZI.

1. **Kila Mwanachuo atavaa sare ya chuo:** -
    a) Aendapo sehemu yoyote mje ya Taasisi na Hospitali
    b) Aendapo kuwakilisha chuo.
    c) Kuonana na walimu/mwalimu ofisini na wodini.
2. Nguo zote za binafsi au za chuo zitakazovaliwa na mwanachuo akiwa ndani na nje ya mipaka ya chuo, lazima ziwe nadhifu zikistahi heshima.
3. Viatu vitakavyovaliwa darasani na sehemu za mazoezi ni rangi nyeusi au kahawia vilivyofunikwa. Viatu vya wazi (open shoes na vyenye visigino vya mbao au misumari) haviruhusiwi kamwe darasani na wodini.
4. Malapa, nguo zenye michoro na maandishi haviruhusiwi katika nafasi za ibada, darasani, au bwaloni. Daima vaa sare ya taasisi kulingana na nafasi husika.

D. KUTEMBEA, KUTEMBELEANA NA LIKIZO ZA DHARURA.

1. Mwanachuo haruhusiwi kulala nje ya chuo isipokuwa kwa kibali maalum.
2. Mwanachuo atakayepewa kibali cha kulala nje sharti arudi wakati alioruhusiwa na aje na barua kutoka kwa wazazi au mlezi.
3. Kutoka nje ya mazingira ya chuo wakati wowote sharti mwanachuo apewe ruhusa kutoka kwababa/mama mlezi wa taasisi, mwalimu wa darasa au mwalimu wa zamu namuda wa kurudi usizidi saa 12kamili jioni.

    4. Taarifa ya Tanzia itolewe na mzazi kupitia namba zifuatazo: **0754-513656, 0689485599**,**0786036141, 0763840456,** na sio kwa mwanachuo.

    5 .Saa za kuwatembelea wanachuo ni**JUMA PILI SAA 10 HADI SAA 12 JIONI**, kwenye **UKUMBI WA TAASISI (RECREATION)**. Wageni wote waandike kwenye kitabu cha wageni. (kama ni dharura) mgeni apitie kwa Mwalimu wa zamu/mlezi wa taasisi.
5. Wageni wa aina yoyote hawaruhusiwi kuingia katika mabweni ya wanachuo.

8. Hatutamruhusu mwanafunzi kutembelea jamaa isipokuwa yule aliyeorodheshwa na mzazi au mlezi kwenye fomu akiwa na sababu maalum. (angalia uk.9)
9. Mwanachuo wa kike haruhusiwi kutembelea Hosteli ya wanachuo wa kiume na hivyo hivyo kwa mwanachuo wa kiume.
10. Hairuhusiwi kupiga picha au kuchukua picha katika mazingira ya taasisi/hospitali bila kibali maalum.

E. MITINDO YA NYWELE NA USAFI.

Mitindo ya nywele inayoruhusiwa kwa wanachuo wa kike:-

A

i. Kusuka mistari ya kurudi nyuma,Kubana nywele kwa nyuma kwa kibanio (cheusi/cheupe)
ii. Kunyoa nywele zilingane

B Mitindo ya nywele inayoruhusiwa kwa wanachuo wa kiume:-

i. Kunyoa nywele zilingane.
ii. Kunyoa ndevu kila mara awapo chuoni.(hairuhusiwi kufuga ndevu)

c. Kucha ziwe fupi kwa wanachuo wote

Usafi na unadhifu vizingatiwe.

F. VYAKULA.

1. Wanachuo hupewa chakula cha kutosha chuoni. Hivyo kamwe mwanachuo asiletewe chakula ndani ya taasisi isipokuwa matunda.
2. Ni marufuku mwanachuo kuhifadhi na kula chakula bwenini (Dormitory)
3. Wanachuo wagonjwa waliolazwa bwenini au hospitalini watapelekewa chakula na wanaohusika.
4. Inabidi kila mwanachuo awahi saa za mlo. Endapo hii haiwezekani basi atoe taarifa mapema kwababa/mama mlezi au mwalimu wa zamu.
5. Heshima wakati wa mlo wowote idumishwe, kelele, fujo ghasia haviruhusiw wakati wa mlo.
6. Kila mwanachuo ahakikishe mahali anapolia chakula panabaki safi. Mabaki ya chakula na maganda ya matunda yawekwe kwenye ndoo zilizowekwa kwa madhumuni hayo.
7. Utunzaji wa vileo na ulevi ni marufuku.
8. Vinywaji visivyo na vileo na matunda vihifadhiwe sehemu iliyotegwa bwaloni.

9. Wageni wasiwemo ndani ya chumba cha mapumziko na bwaloni wakati wa mlo pia asishiriki chakula cha wanachuo.

G. UTUNZAJI WA VIFAA, MAZINGIRA NA MALI YA CHUO.

Taasisi/Hospitali na vifaa vyake ni mali ya umma wa leo na kesho, hivyo kila mmoja anawajibika kuitunza mali hiyo.

1. Kila mwanachuo atakabidhiwa vifaa muhimu ambavyo atavitumia, kuvitunza na kuvikabidhi kabla ajaondoka chuoni. Mwanachuo haruhusiwi kuhamisha kifaa chochote kutoka mahali kilipo na kukipeleka mahali pengine bila ruhusa maalum.
2. Mwanachuo anapoharibu kifaa cha taasisi au hospitali, sharti atoe taarifa kwa muhusika kulingana sehemu husika.
3. Akipoteza, kuvunja au kuharibu kifaa chochote – AtakilipaNi marufuku kwa mwanachuo kutumia vifaa vya kufundishia kama chaki, ubao vyumba vya mazoezi (SKILLS LABORATORY) computer room n.k bila ruhusa ya mwalimu wa somo.
4. Ni marufuku kuchukua vitabu bila idhini ya mkutubi(librarian) na vitabu vilivyoazimwa virudi katika hali nzuri na kwa muda uliopangwa

5. **<u>Ni marufuku kutupa vigae vya chupa, vioo, plasitiki, viatu, makokwa ya matunda katika shimo la kuchomea taka, viwekwe kwenye pipa maalumu kwa ajili hiyo na visifungwe kwenye mifuko ya lambo</u>**
6. Vyoo vitunzwe katika hali ya usafi, tumia vyoo vya nje wakati wa mchana na vyoo vya ndani wakati wa usiku. Tumia karatasi laini (toilet paper) unapotumia vyoo vya ndani.
7. Matumizi ya maji: Funga bomba wakati wote lisipotumika na bomba zinazovuja au kuharibika, ripoti itolewe mara moja kwa mhusika. (Warden)
8. Vitambaa vya kujihifadhi (sanitary pads) vichomwe kwenye tanuru (incinerator)
9. Utunzaji wa Vyumba: Hairuhusiwi kuchora, kugonga misumari, kubandika, au michoro ya aina yoyote ukutani.
10. Utunzaji wa kitanda: Hairuhusiwi kukalia kitanda, kuweka mapambona vitu uvunguni.Kitanda kifunikwe na shuka la blue (Bed Cover)
11. Viatu viwesafi na vitunze kwenye sehemu iliyotengewa shughuli hiyo.

H. HESHIMA NA MAWASILIANO.

1. Yampasa mwanachuo kutii na kuwaheshimu wafanyakazi wote wa chuoni na hospitalini, viranja na wanachuo wenzake pamoja na wagonjwa na jamaa zao.
2. Si adabu ukiwa ndani ya mazingira ya taasisi kuzungumza/kuongea na watu walioko njeya uzio (gate)
3. Mwanachuo unapaswa kusaidiana na kushirikiana na wanachuo wenzako wote katika mambo yote mema na halali kwa mujibu wa kanuni hizi:- sheria za Mungu, sheria za nchi na maadili ya watoa huduma wa afya.
4. Lugha ya mawasiliano ni Kiingereza wakati wote. Kiswahili kitumike wakatiwa kuhudumia wagonjwa.

AFYA

1. Kila mwanachuo anayeanza mafunzo, sharti awe na afya nzuri. Afike na fomu ya Afya na iwe na muhuri wa Hospitali inayotambulika.
2. Mwanachuo hataruhusiwa kuendelea na masomo akiwa na afya dhaifu kiasi cha kushindwa kuhudhuria masomo darasani na wodini.
3. Mwanachuo atakapo umwa sharti atoe taarifa kwa mwalimu muangalizi wa afya za wanachuo,mwalimu wa zamu,baba/mama mlezi na mwalimu wa darasa.

Mwanachuo haruhusiwi kutunza dawa iwe ya hospitali au ya asili bila idhini ya waliotajwa hapo juu.

4. Mwanachuo haruhusiwi kuchukua mapumziko ya kuumwa (ED) hata kama yameidhinishwa na Daktari pasipo mwangalizi wa wagonjwa/mlezi au mwalimu wa zamu kufahamu.

5. Siku za kuugua au kuwa nje ya taasisi zikizidi 21 kwa miaka 3, 14 kwa miaka 2 na 7 kwa mwaka 1,sharti mwanachuo arudie muhula ili aweze kufanya mtihani wake wa mwisho

6. Uvutaji wa sigara, Bangi na ulevi haviruhusiwi chuoni

7. Wanachuowa kike watapimwa afya zao mara mbili kwa mwaka.

I. MAAGIZO MENGINE.

1. Mwanachuo aendapo likizo inabidi aende nyumbani kwa mzazi/ mlezi au mfadhili wake.

2. Mzazi/ Mlezi/ Mfadhili anatakiwa ampatie mwanae vifaa vya kutosha kama nguo za heshima, sabuni, kalamu, daftari, mifuto, rula n.k. Hairuhusiwi wanachuo kupeana au kuazimana nguo. Hili si jambo jema wala si la afya.

3. Mwanachuo hutazamiwa kufuata maadili ya dini yake kikamilifu awapo chuoni, hivyo atapatiwa nafasi na muda wa sala, kama ifuatavyo: Saa za kusali ni 12:15 alfajiri, saa 1:30 asubuhi na saa 4:30 usiku. Pia kila mwanachuo aje na vifaa vya sala kadiri yadhehebu lake. Kama ilivyoandikwa katika fomu ya vifaa.

4. Hali ya ukimya udumishwe baada ya kutimia saa za kulala (saa 5.00 usiku). Vile vile si vyema kuwapigia kelele wanachuo ambao wametoka zamu za usiku wakiwa wamelala mabwenini.

J.SHERIA ZA TAASISI

No	SHERIA	MARA YA MWANZA	MARA YA PILI	MARA YA TATU
1	Maendeleo mabaya ya TAALUMA yake			
2	**KUGUSHI MITIHANI, Vyeti na Nyaraka za wagonjwa n.k.**	Kuandika barua/Kusitisha masomo kwa muda/Kufukuzwa chuoni		
3	Kumtukana au kumpiga Mwalimu, Mlezi,Daktari,Muuguzi,Mfanyakazi, mwanafunzi mwenzako, wagonjwa na jamaa za wagonjwa	Kuandika barua ya onyo	Kusitisha masomo kwa muda	Kufukuzwa chuo
4	Kuvunja maadili ya watoa huduma wa afya kiasi cha kuvunja hadhi na kuhatarisha usalama wa mgonjwa, jamaa, wewe mwenyewe, hospitali na chuo	Kuandika barua ya onyo	Kusitisha masomo kwa muda	Kufukuzwa chuoni
5	Kugoma, kusababisha/kuchochea mgomo, ghasia na uzushi.	Kufukuzwa chuoni		
6	Wizi, ulevi wa aina yeyote, mwenendo wa kiasherati.	Kuandika barua ya onyo/Kusitisha masomo kwa muda	Kusitisha masomo kwa muda	Kufukuzwa chuoni
7	Kuharibu kwa kukusudia mali ya chuo, hospitali,wagonjwa na mwanafunzi mwenzako.	Kuandika baua ya onyo/Kulipa kifaa	Kulipa/Kusitisha masomo kwa muda	Kufukuzwa chuoni
8	Kuzuzua mwenzako	Kuandika barua	Kusitisha masomo kwa muda	Kufukuzwa chuoni
9	Kubeba mimba, kuharibu mimba, jaribio la kutaka kuolewa au kumpa mwanachuo mwenzako mimba, kukutwa na vidonge vya kuzuia mimba na kondomu	Kurudia mwaka wa masomo/Kusitisha masomo kwa muda	Kufukuzwa chuoni	
10	Utoro wa aina yoyote.	Kuandika barua	Kusitisha masomo kwa muda	Kufukuzwa chuoni

K: MATUMIZI YA SIMU,LAPTOP NA TABLET.

A:SIMU

I. Simu zinaruhusiwa chuoni kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano.Simu hizo haziruhusiwi kutumika katika maeneo yafuatayo:-darasani,wodini na sehemu za ibada.

II. Maongezi ya simu hayaruhusiwi bwenini tumia ujumbe mfupi wa maneno (sms).

III. Simu zichajiwe sehemu maalumu iliyotengwa kwa ajili hiyo ambazo ni: darasan(private study)i,recreation,sehemu ya kunyooshea nguo, na sehemu ya kufulia nguo.

B: LAPTOP/TABLET

I. Laptop/tablet zinaruhusiwa chuoni kwa ajili ya masomo,mazoezi ya darasani(assignments). Laptop/tablet hizo haziruhusiwi kutumika katika maeneo yafuatayo:-darasani kama kuna mwalimu,wodini na sehemu za ibada.

II. Laptop/tablet zichajiwe sehemu maalumu iliyotengwa kwa ajili hiyo ambazo ni: darasan(private study)i,recreation,sehemu ya kunyooshea nguo, na sehemu ya kufulia nguo.

III. Wakati wa mitihani hairuhusiwi kuingia na simu/laptop/tablet.

IV.

N:B: **Taasisi haitahusika na upotevu wa laptop/tablet au simu ya mwanachuo.**

K. UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI MWANAO AWAPO CHUONI WAKATI WA DHARURA, ATAWASILIANA NA JAMAA WAFUATAO

JINA KAMILI	ANUANI YAKE/SIMU	UHUSIANO
1.	....	....
2	....	....
3	....	....

MIMI .....

ANUANI NA SIMU .....

Nathibitisha waliotajwa hapo juu kuwa ni ndugu na jamaa zangu wa karibu, pia nimezisoma kwa uangalifu kanuni hizi pamoja na mwanangu amekiri mbele yangu kuwa anazikubali na atazifuata kikamilifu.

Saini ya Mzazi / Mlezi/ Mfadhili: .....

Tarehe: .....

Saini ya mwanachuo .....

Tarehe .....

Jina la aliyempokea .....

Saini ya aliyempokea .....

Tarehe .....

PRE-SERVICE CANDIDATES IMPORTANT INFORMATION

THIS FORM MUST BE COMPLETED BY A CANDIDATE AND PARENT/GUARDIAN.

A: PERSONAL PARTICULARS.

1. FULL NAMES
   .....
2. SEX: .....
3. DATE OF BIRTH: .....
4. RELIGION: .....
   (specify) RC, /LUTHERAN, Anglican,Shir, Bakwata Others .....
5. NATIONALITY .....
6. TRIBE .....
7. VILLAGE/STREET

B: CONTACT ADDRESS

Father: Name……..
Address……PhoneNo.……

Mother: Name: ……..
Address …….. Phone No. ……..
Guardian: Name: ……..
Address ……Phone No. ……

C: SOCIAL INTERESTS:

What are your hobbies?
.....
.....
.....

D: (i) list your nearby relatives in Muleba District/Kagera Region

Name	Relationship	Phone no/ Address
1.	.....	.....
2.	.....	.....
3.	.....	.....

(ii) Who will pay your fees?

Name	Relationship	Occupation	Phone No
1.	.....	.....	.....
2.	.....	.....	.....
3.	.....	.....	.....

E.HEALTH HISTORY

a) Do you have chronic illness? (Yes/No) if yes mention them.
   1. .....
   2. .....
   3. .....

b) Have you ever undergone any major operation? If so mention them:-

   Type of operation ..... Year .....
   Indication .....
   Hospital .....

c) Do you have any complication as a result of operation done? If so mention them.
   1. .....
   2. .....
   3. .....

d) Any other health problems:
   .....
   .....
   .....

Filled in by: Name .....
Signature ..... Date.....

RUBYA HEALTH TRAINING INSTITUTE

P.O.BOX 133, RUBYA – BUKOBA - TANZANIA
Email: info@rhti.ac.tz , Website: www.rhti.ac.tz,
Mobile: +255 766 209 213, +255 786 594 733, +255 754 513 656, +255

S/No.	A: KARO	CO. & LAB 1	CO. & LAB 2	CO. & LAB 3	NURSE 1	NURSE 2	NURSE 3	COMMUNITY	DISTANCE LEARNING 1	DISTANCE LEARNING 2	MIDI-WIFERY
		DIP & CERT	DIP & CERT	DIPLOMA	DIP &CERT	DIP &CERT	DIPLOMA	HEATH	DIPLOMA	DIPLOMA	BRIDGE
	TUITION	1,500,000	1,400,000	1,400,000	1,200,000	1,200,000	1,200,000	1,000,000	900,000	900,000	500,000
	CHAKULA	600,000	600,000	600,000	600,000	600,000	600,000	600,000			
	JUMLA. 'A'	**2,100,000**	**2,000,000**	**2,000,000**	**1,800,000**	**1,800,000**	**1,800,000**	**1,600,000**	**900,000**	**900,000**	**500,000**
	B: MICHANGO MINGINE										
1	Medical Capitation	20,000	20,000	20,000	20,000	20,000	20,000	20,000			
2	Skills Laboratory	45,000	40,000	40,000	40,000	50,000	50,000	50,000	35,000	35,000	50,000
3	Mitihani ya ndani NTA level 4 -6	260,000	200,000	220,000	190,000	300,000	300,000	200,000	200,000	200,000	
4	ITHIBATI YA CHUO	150,000	150,000	150,000	150,000	150,000	150,000	150,000			
5	Internet fee	20,000	20,000	20,000	20,000	20,000	20,000	20,000			
6	Stationery	230,000	180,000	200,000	140,000	210,000	250,000	170,000			70,000
7	Kitambulisho + picha	10,000			10,000			10,000			
8	Matumizi ya maji	60,000	60,000	60,000	60,000	60,000	60,000	60,000			
9	Matumizi ya umeme	80,000	80,000	80,000	80,000	80,000	80,000	80,000	20,000	20,000	40,000
10	Ukarabati mdogo	50,000	80,000	80,000	50,000	80,000	80,000	50,000			40,000
11	Hostel	120,000	120,000	120,000	120,000	120,000	120,000	120,000			
12	Vitabu vya mazoezi/procedure books	40,000	40,000		20,000	40,000		50,000	70,000		60,000
13	Usajili wa chuo NACTE	15,000			15,000			15,000	15,000	15,000	15,000
14	Registration TNMC (Diploma)									80,000	
15	Final nursing midwifery Examination										150,000
	JUMLA YA KARO. 'B'	**1,100,000**	**990,000**	**990,000**	**915,000**	**1,130,000**	**1,130,000**	**995,000**	**340,000**	**350,000**	**425,000**
	JUMLA YA KARO A+B	**3,200,000**	**2,990,000**	**2,990,000**	**2,715,000**	**2,930,000**	**2,930,000**	**2,595,000**	**1,240,000**	**1,250,000**	**925,000**

UTARATIBU WA MALIPO NI KAMA IFUATAVYO:-

AWAMU	CO.1 & LAB 1	CO.2 & LAB 2	CO. & LAB 3	NURSING 1	NURSING 2	NURSING 3	COMMUNITY	DS. LEARNING 1	DS. LEARNING 2	MIDI-WIFERY
	DIP & CERT	DIP & CERT	DIPLOMA	DIP &CERT	DIP &CERT	DIPLOMA	HEATH	DIPLOMA	DIPLOMA	BRIDGE
Kujiunga na chuo (muhula wa 1)	1,200,000	1,000,000	1,000,000	1,000,000	1,000,000	1,000,000	900,000	700,000	700,000	500,000
Kabla ya CAT II/Test II (Muhula wa I)	400,000	495,000	495,000	465,000	465,000	465,000	450,000	300,000	300,000	225,000
Kujiunga na muhula wa II	1,200,000	1,000,000	1,000,000	800,000	1,000,000	1,000,000	800,000	240,000	250,000	200,000
Kabla ya CAT II/Test II (Muhula wa II)	400,000	495,000	495,000	450,000	465,000	465,000	445,000			
JUMLA	**3,200,000**	**2,990,000**	**2,990,000**	**2,715,000**	**2,930,000**	**2,930,000**	**2,595,000**	**1,240,000**	**1,250,000**	**925,000**

MALIPO HAYA YAPITIE KATIKA AKAUNTI ZIFUATAZO:-

1. CRDB A/C NO. **0150522419300** Tawi la Muleba
2. NMB A/C NO. **32003500034** Tawi la Muleba

JINA LA AKAUNTI : RUBYA HEALTH TRAINING INSTITUTE

N.B Mzazi/Mfadhili utampatia mwanachuo/mwanao yafuatayo:-

i) Pesa ya matumizi binafsi

ii) Pesa ya BIMA ya Afya (NHIF) Tshs 50,400/= kama mwanachuo atakuwa hana BIMA ya Afya au BIMA aliyonayo inakaribia kuisha muda wake.

iii) Sare ya chuo Tshs 160,000/= Ikijumuisha uniform mbili (2) T- shirt (2) sweta (1) kizibao (1) cha kuvaa wodini hii ni kwa Wauguzi na Afya ya Jamii na Koti (1) hii kwa watabibu na maabara.

iv) Umoja wa wanachuo (Students' Union) Tshs 10,000/=

v) Mchango wa mahafari Tshs 30,000/= kwa mwanachuo anayehitimu.

vi) Pesa kwa ajili ya usahishaji wa mtihani Tshs 280,000/=, pesa hii italipwa kwa KATIBU MKUU Wizara ya Afya,Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Kabla ya January 9, 2018.

kwenye akaunt zifuatazo:-

1. NMB A/C NO. **20110007946** NMB BANK HOUSE

Jina la akaunt "Application and Examination Fee"

Andika Examination fee ya.....(Jina la mwanachuo) wasilisha **Bank Pay-In-Slip** chuoni

vii) Pesa za utafiti (Research)

(1) Tshs 220,000/= Afisa tabibu na Maabara mwaka wa pili pamoja na Uuguzi stashahada mwaka wa tatu

(2)Tshs 150,000/= Hii ni kwa Uuguzi Stashahada na Cheti mwaka wa pili.

(3) Tshs 120,000/= Somo la Ustawi wa jamii - vitendo (COMMUNITY HEALTH)

viii) Usajili TNMC Tshs 80,000/= Uuguzi ngazi ya STASHAHADA na 60,000/= ngazi ya cheti

xi) Mental Health Tshs 100,000/= hii ni kwa E- LEARNING mwaka pili na stashahada mwaka wa tatu (Afya ya akili)

.....

DR. FR. FELIX KAMUGISHA

MKUU WA TAASISI

RUBYA HEALTH TRAINING INSTITUTE (RHTI)
PRINCIPAL
S.L.P.133
RUBYA -BUKOBA

RUBYA HEALTH TRAINING INSTITUTE
P.O. BOX 133,
RUBYA – BUKOBA.

MEDICAL CERTIFICATE FOR APPLICANTS OF PRE-SERVICE CERTIFICATE, DIPLOMA AND ONE YEAR COURSE OF COMMUNITY HEALTH

Dear Doctor

Please examine Mr. /Ms .....
Who is seeking admission for the .....Pre-services Course and certify whether he/she is physically and mentally fit to undergo the stated above course without hindrance within one year/ two years/ three years course of studies. Specify if any chronic health problem is identified which needs special attention.

.....
PRINCIPAL

RUBYA HEALTH TRAINING INSTITUTE (RHTI)
PRINCIPAL
S.L.P.133
RUBYA-BUKOBA

Date .....

Name of hospital .....

B/P ..... VDRL ..... Urine for sugar .....
Urine for pregnancy test (female) .....

I certify that I have physically examined Mr. /Ms ..... and found that the applicant is **fit / not fit** to undergo the stipulated course without hindrance.
.....
.....
.....
.....

Other remarks
.....
.....
.....

Name ..... Signature
.....
Designation .....Date
.....

Official stamp.